



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HWT/L17/75

02.05.2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anakaribisha maombi ya Ajira za Mkataba Kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.

DEREVA DARAJA LA II NAFASI (04)

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kuendesha gari la abiria na malori
- ii. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- iii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftali la safari.
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadili utakavyoelekezwa na Mwajiri wako.

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mtanzania mwenye cheti cha kuzaliwa na kitambulisho au namba ya kitambulisho cha Taifa (**NIDA**)
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na lesen ya Udereva daraja C
- iii. Awe na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitano (5) bila kusababisha ajali.
- iv. Awe na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II au sifa nyingine inayolingana nayo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- v. Awe na umri wa **miaka 18** au zaidi na asiwe na *umri unaozidi miaka 45*.
- vi. Awe na afya njema, mchapa kazi na mwenye utayari wa kufanya kazi udereva katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime.

2 NAMNA YA KUOMBA


- a) Maombi yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Kijiji Cha Nyamwaga, Barabara ya Nyamwaga, S.L.P 16, Tarime-Mara, Simu +25528-2690518, Nukushi: +25528-2690144, Barua pepe: ded@tarimedc.go.tz, Tovuti: www.tarimedc.go.tz.
- b) Maombi yote yatumwe na kuambatisha nakala za vyeti vya taaluma, mafunzo, cheti cha kuzaliwa, na Kitambulisho cha Taifa vilivyothibitishwa na Mahakama au na mtu yeyote aliyeidhinishwa na Serikali.
- c) Maombi yatakayo ambatishwa na Testimonials' 'Provisional Results', Statement of Results; Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita **HAYATAFANYIWA KAZI**.
- d) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kishwahili au kingereza tofauti na hapo maombi hayatafanyiwa kazi.
- e) Waombaji watakaobainika kwa kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- f) Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (detail CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.

3.1. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Maombi yatapokelewa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Nyamwaga, mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **12.05.2023** saa **9:30** alasiri.

Tunawakaribisha wote wenye sifa zilizotajwa hapo juu kuwasilisha maombi yao kwa utaratibu ulioelekezwa. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ya:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 16,
TARIME.**


Solomon I. Shati
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
TARIME.**
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

Nakala:

Tangazo hili lkinapatikana kwenye mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pamoja na kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambayo ni: www.tarimedc.go.tz.

Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Kijiji Cha Nyamwaga, Barabara ya Nyamwaga, S.L.P 16, Tarime-Mara, Simu +25528-2690518, Nukushi: +25528-2690144, Barua pepe: ded@tarimedc.go.tz, Tovuti: www.tarimedc.go.tz